



## JARIDA LA MBEGU



Toleo. 69 May 2003 Tafsiri Julai 2005

### *Khaya anthotheca* (Welw.) C.D.C

#### Jamii na utaratibu wa majina

**Jamii:** Meliaceae

**Majina mengine:** *Garretia anthotheca* Welw.; *Khaya nyasica* Stapf ex Baker f.; *K. agboensis* A. Chev.; *K. euryphylla* Harms.

**Kienyeji/majina ya kawaida:** (East) African mahogany, Uganda mahogany, white mahogany, grand bassam mahogany (Eng.); acajou blanc, acajou d'Afrique (Fr.); krala (trade name).

**Jamii nyingine zilizo karibu:** *Khaya anthotheca* kwa mara nyingi hulinganishwa na *K. grandifolia* hata hivyo sio rahisi kutambua tofauti kati ya jamii hizi mbili. Katika makala na vitabu fulani *K. nyasica* hutofautishwa na *K. anthotheca* lakini wataalam wengi hukubali kwamba miti hiyo ni ya jamii moja.


#### Maenezi

Huu ni mti uliotokea katika sehemu za hari ya Afrika kati ya 20°S na 10°N, kutoka Sierra Leone mashariki hadi Uganda na Tanzania na kuelekea kusini hadi Angola, Zambia, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe lakini haupatikani katika sehemu baridi za nyanda ya juu na chini mwa Guinea mahali ambapo jamii ya *Khaya ivoriensis* ndio hupatikana. Mti huu pia hupatikana katika nyanda za chini na kwenye mito na sehemu za mwinuko wa 1500m, na viwango vya mvua 600-1600mm kwa mwaka.

Katika maeneo ya mandhari hai, mti huu hupandwa kwa wingi. Mti huu umefaulu sana katika nchi ya Afrika Kusini, Cuba na Puerto Rico na kwa kiwango kidogo kule Indonesia na Malaysia mahali ambapo mti huu umetumiwa katika mfumo wa *Tangya*.

Mti huu hutumiwa kwa wingi na umeenea sana katika Afrika ya Mashariki na Magharibi. Katika maeneo yasiyo na miti mingi, nasaba za kizazi cha mti huu hukisiwa kuwa na kasoro. Mataifa mengi yamepiga marufuku ukataji wa mti huu na usafirishaji pia umekomeshwa. Katika orodha ya mwaka wa 2002 ya IUCN, huu ni mojawapo ya

miti iliyotiwa mstari mwekundu kwa kukabiliwa na tisho la kuangamia.



1, Tawi la maua; 2, ua la kike; 3, ua la kiume; 4, tunda kavu, sehemu moja imeondolewa. Kutoka: Miti ya Nchi za Hari katika Afrika Mashariki. Mchoraji Julia Loken.

#### Matumizi

Huu ni mojawapo ya mti maarufu kwa kutoa mbao katika Afrika. Huu ni mti unaotumiwa kutengeneza bidhaa za hali ya juu kama vile kabati na pia ubao mwembamba wa kubandika ubao usio mzuri, au panapohitaji ya mbao za kudumu. Uzito wake kwa kiwango cha unyevu wa 12% ni 620kg/m<sup>3</sup>. Mbao zake ni za rangi nyekundu na madoa ya kuvutia, ngumu, lakini huchukua rangi kwa urahisi. Huu ni mti unaokauka vyema na haushambuliwi na wadudu wa kupekecha au mchwa. Gome lake hutumiwa kama dawa ya kuzuia kikohozi na homa. Mti huu ni maarufu sana kwa kutoa kivuli bora na shughuli za kurembesha mazingira, na aidha kuzuia upepo mkali.

#### Jarida la Mbegu:

<http://www.sl.kvl.dk/Publikationer/Udgivelser/PopulaerPublikationer/DFSCSL69.aspx>

Sakura = "seed leaflets"

### **Maelezo ya ukuaji**

Huu ni mti mkubwa, kufikia urefu wa 60m, shina lililo imara refu na lisilo na matawi hadi tu kileleni. Shina hili huonekana kama lililochibuka kwa umbali hadi urefu wa 6m. Juu ya sehemu hiyo shina hilo ni la mduara wa had 4m. Majani hufikia urefu wa 40cm, kwenye makundi, na vijitawi kama ubawa kufikia 6-10, kila kijitawi kufikia urefu wa 17cm.

Maua ni ya kiume na kike kwa pamoja, yenye harufu nzuri na meupe, kwenye chana la urefu wa 40cm. Maua ya kike na kiume yako kwenye mti mmoja (*monoecious*), maua hayo hufanana ila tu aina moja ya kiungo hukosa kufanya kazi iwapo ile nyingine imekomaa kwa wakati mmoja.



Mbegu za *K. anthothea* zilizo ota. Picha: Kirsten Thomsen, DFSC

### **Matunda na mbegu**

**Tunda:** tunda ni la rangi ya hudhurungi, kavu, ngumu, mduara wa 4-6cm, lenye sehemu 4-5. Kuna jumla ya mbegu 40kwa kila sehemu. Mbegu zimejipanga kutokea pale katikati.

**Mbegu:** rangi yake ni ya hudhurungi, 1-2 x 1.5-3cm, nyembamba na kuzungukwa na ubawa mwembamba. Kuna takriban mbegu 2000-4000 kwa kila kilo moja.

### **Maua na kuota matunda**

Mti huu huota maua mwishoni mwa kipindi cha kiangazi au mwanzoni mwa msimu wa mvua, hasa mwezi wa Novemba, na matunda kukomaa mwezi wa Machi hadi Julai au baadaye. Maua huchavuliwa na wadudu, huku mbegu zilizo na ubawa zikitawanywa na upepo.

### **Mavuno**

Punde tu mbegu zinapokomaa, tunda lile hupasuka. Matunda ambayo hayajapasuka au yanayo onyesha dalili ya kupasuka huchunwa kutoka kwa mti. Wakati wa kuvuna mbegu, kiwango cha unyevu ni 10-15%.

### **Matayarisho na utunzaji**

Matunda hayo hukaushwa kwenye jua hadi pale yanapokauka na kupasuka, kisha mbegu huchukuliwa. Mbegu hizo hukaushwa kwenye jua.

### **Hifadhi na uwezo wa kumea**

Mbegu hizi hazitakauka sana, hata hivyo jaribu kufikisha kiwango cha unyevu kilicho chini (5-7%) na kuhifadhi kwenye vifuko au kitu kisicho pitisha hewa. Utafiti umebainishwa kwamba mbegu hizi hazifai kuwekwa kwenye viwango vidogo vya joto, kiwango kifaacho ni 15°C wala sio 5 au -18°C, lakini uchunguzi huo sio bayana. Iwapo mbegu zimekaushwa vyema, uwezo wa kumea hudumishwa hadi miezi 6 na kupungua baada ya mwaka. Mapendekezo ni kupanda mbegu katika kipindi cha mwaka mmoja baada ya mavuno.

### **Matayarisho ya upanzi**

Mbegu hizi hazitahitaji matayarisho maalum kabla ya kupanda.

### **Kupanda na kuota**

Mbegu ambazo hazijahifadhiwa kwa muda mrefu hukua kwa viwango vya 60-90%. Mbegu huota kwa kutoa majani mawili (ambayo hubaki kwenye mchanga), na hukua kwa asilimia 20% baada ya wiki moja na kujitokeza kwa kikamilifu wiki tatu baada ya kupanda.

Katika Afrika ya Kusini, matokeo bora hupatikana kwa kupanda mbegu kwenye kiunga kilicho na mchanga uliochanganywa na sehemu ya gome la mti wa *pine* kwa pamoja na boji. Kupanda mbegu kwenye kiunga hufanya vyema kuliko kupanda kwenye vifuko. Viunga vyapaswa kupewa kivuli na maji ya kutosha. Punde tu miche inapofikia urefu wa 5cm ng'oa na kupanda kwenye vifuko kisha baada ya mwaka mmoja, miche inapofikia urefu wa 30cm ni tayari kuatika. Licha ya matokeo bora kutokana na upanzi kutoka kwa mbegu, vipandikizi vimetumiwa na kuonyesha matokeo bora. Waweza pia kung'oa miche kutoka kwenye misitu au eneo lililo na miti hii kwa wingi. Baadhi ya

miche hupindika na shina kujikunja, miche kama hii haitumiwi. Hata hivyo upanzi wa kutumia vipandikizi haujafanyiwa majaribio sana.

Baada ya kupanda miche, utahitajika kupalilia mara kwa mara kukabili kwekwe na nyasi. Mti huu haufanyi vyema baada ya kukatwa.

### **Marejeleo na majarida mengine**

**Bussche, G.H. von dem 1982.** *The establishment of hardwood plantations for the production of furniture and joinery timber in the Transvaal.* South African Forestry Journal, 121.

**IPGRI/DFSC 1998.** *The Project on Handling and Storage of Recalcitrant and Intermediate Tropical Forest Tree Seeds.* Newsletter no. 4. International Plant Genetic Re-source Institute/Danida Forest Seed Centre.

**IUCN 2002.** *2002 IUCN Red List of Threatened Species.*

**Msanga, H.P. 1998.** *Seed Germination of Indigenous Trees in Tanzania.* UBC Press, Vancouver, BC.

**Palgrave, K.C. 1977.** *Trees of Southern Africa.* Struik Publishers, Cape Town.

**Soerianegara I., R.H.M.J. Lemmens, eds., 1993.** *Plant Resources of South-East Asia No. 5(1). Timber trees: major commercial timbers.* PROSEA. Bogor Indonesia.

MAKALA HAYA YALITAYARISHWA KWA  
USHIRIKIANO NA KITUO CHA MBEGU ZA MITI  
NCHIN TANZANIA

**Mwandishi: Dorte Jøker, DFSC**

### **Majulisho:**

*Tafsiri:*

**Patrick Bunyali Kamoyani**

Email: [pbkamoyani@lycos.co.uk](mailto:pbkamoyani@lycos.co.uk) au [pbkamoyani@excite.com](mailto:pbkamoyani@excite.com)

Forest & Landscape Denmark	Simu: +45-35 28 15 03
Hørsholm Kongevej 11	Kipepesi: +45-35 28 15 17
DK-2970 Hørsholm Denmark	Barua-pepe: <a href="mailto:SL-International@kvl.dk">SL-International@kvl.dk</a>
	Mtandao: <a href="http://www.SL.kvl.dk">www.SL.kvl.dk</a>